# TNMC Habari

Toleo No. 0014

TOLEO MAALUMU

Oktoba, 2024

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari




**Ujenzi wa Ofisi za TNMC Dodoma Wafikia 63%**

Habari Uk. 05



**TNMC yazindua Namba Mpya ya Huduma kwa Wateja.**

Habari Uk. 06




## Waziri Mhagama Kushughulikia Hoja za Wauguzi



Habari Uk. 01

## Mitaala ya Uuguzi na Ukunga, Famasia, Fiziotherapia, Yajadiliwa Kwenye Kamati za Bunge

Habari Uk. 02

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**

Bi. Agnes Mtawa

**MHARIRI**

Mwakapiso Ndimmyake

**WARATIBU**

Irene Chilewa
Rose Mhando

**MSANIFU JARIDA**

Ezekiel Nyalusi

P.O BOX1736 DODOMA

@tnmchabari www.tnmc.go.tz Info@tnmc.go.tz

# Waziri Mhagama Kushughulikia Hoja za Wauguzi.



**Na. Mwandishi Wetu.**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama Oktoba 17, 2024 amekutana na Uongozi wa Chama cha Wauguzi na Ukunga Tanzania (TANNA) na kujadili mpango kazi wa utekelezaji wa hoja za wauguzi zilizo jitokeza wakati wa mkutano wa mwaka uliofanyika 12 Mei, 2024 ili kuongeza ubora wa Huduma kwa wananchi.

Mhe. Mhagama amesema kuwa anatambua mchango na kazi kubwa inayofanywa na wauguzi na wakunga katika sekta ya afya hivyo anawapongeza kwa kazi nzuri inayofanyika katika kuwahudumia wananchi.

Amesema moja ya jukumu kubwa analofanyia kazi kwa sasa ni kuhakikisha wauguzi na wakunga wanapandishwa madaraja kama ilivyo kwa kada zingine.

***"Wakati tunafanyia kazi changamoto zenu tusaidieni kusimamia maadli kwa wauguzi ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi",*** ametoa rai Mhe.Mhagama.

Amesema serikali kupitia wizara ya Afya inafanya kazi kuhakikisha inatatua changamoto wanazokabiliana nazo wauguzi na wakunga hivyo waendelee kuchapa kazi kwa kufata miiko na maadili ya taaluma wanapo wahudumia wananchi.

Kwa upande wake rais wa Chama cha Wauguzi na Ukunga Tanzania (TANNA), Alexender Baluhya amesema kuwa wauguzi na wakunga wanaimani na serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassani kuwa ni sikivu na itatatua changamoto zao kwa wakati ili kuleta tija katika utendaji kazi wao.

Amefafanua kuwa lengo la kukutana na Mhe.Mhagama ni kufatilia utekelezaji wa hoja za wauguzi zilizotolewa katika mkutano wa mwaka uliofanyika pale Mkoani Tanga- na hoja hizo ikiwemo kupandishwa madaraja.



# Mitaala ya Uuguzi na Ukunga, Famasia, Fiziotherapia, Yajadiliwa Kwenye Kamati za Bunge



**Na. Mwandishi Wetu**

Kamati za Kudumu za Bunge zinazohusika na masuala ya afya na elimu zimetoa rai kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya kushirikiana na Wadau wa kisekta katika kuboresha mitaala mipya ya kada za Uuguzi na Ukunga, Famasia na Fiziotherapia.

Rai hiyo imetolewa Oktoba 18, 2024 kwenye kikao kilichozikutanisha kwa pamoja Kamati ya Bunge za Afya na Masuala ya Ukimwi pamoja na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo na Viongozi na Wataalam kutoka Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu.

Kamati hizo zimeshauri Wizara ya Afya kushirikiana na Wadau kwa kuzingatia kanuni, taratibu za Mabaraza za uandaaji wa mitaala. Aidha Kamati imeitaka Wizara ya Afya kuandaa vikao vya kuwaelimisha wadau katika vikao husika kuhusu uhusiano uliopo baina ya vigezo na maudhui yaliyopendekezwa kwenye mitaala.

Akizungumza kwa Niaba ya Wazri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema Serikali itaendelea kuwashirikisha na kuwaelimisha wadau katika hatua mbalimbali za usimamizi na uendeshaji wa mafunzo kwa maslahi mapana ya Taifa katika kulinda na kuboresha huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi.

***"Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaandaa vikao vya wadau wa mitaala ya mafunzo kwa kila mtaala ili kupata maoni yao yatakayosaidia kufanya maboresho ya mitaala hiyo"*** amesema Dkt. Mollel.

Dkt. Mollel amebainisha kuwa Wizara imejipanga kusambaza mitaala mipya iliyohuishwa kuanzia kipindi cha Julai 2025 hadi Septemba 2025 ili iweze kuanza kutumika kwenye mwaka wa masomo 2025/2026 utakaoanza mwezi Oktoba,2025.



# Wauguzi, Wakunga wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe Wapigwa Msasa Namna ya Kutunza Chumba cha Upasuaji.

Na. Mwandishi wetu



Watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe wanaofanya kazi katika Idara ya Upasuaji wamenufaika na mafunzo kuhusu huduma za upasuaji, ili kuongeza ufanisi na kuimarisha ubora wa huduma katika Idara hiyo.

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa na Mtaalamu Bi. Salome Kassanga kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) yalianza tarehe 15, Oktoba na kutamatika tarehe 28, Oktoba 2024, na hivyo kukamilisha wiki mbili za mafunzo.

Mafunzo yamehusisha Madaktari, wauguzi, wakunga na wataalamu wa Dawa za Usingizi na ganzi.
Akizungumza wakati wa utoaji wa Mafunzo Bi. Kassanga amewataka wauguzi, wakunga na wataalamu wa chumba cha upasuaji kuzingatia yale waliyojifunza ili kuhakikisha wanazuia maambukizi katika chumba cha upasuaji.

Naye Mkuu wa mkoa wa Njombe Mhe. Antony Mtaka amepongeza juhudi za Baraza kutoa mafunzo hayo huku akiitaka wizara ya Afya kufanya tafiti zaidi ya kujilidhisha kwanini vifo vya akina mama vinaongezeka baada ya kujifungua.

***“ipo haja ya Wizara ya Afya kufanya tafiti kwanini vifo vya kutoka wakati wa kujifungua mpaka baada ya kujifungua, tumekuwa na kesi nyingi za namna hiyo siyo tu Njombe nimeona hata mitandaoni, hata katika familia zetu tunaona mama anajifungua salama ila ndani ya kipindi cha siku kumi mama anaanza kubadilika hali mpaka anapoteza maisha ni muhimu kama wadau wa Afya kulifanyia tafiti suala hili”***

Kwaupande Afisa Muuguzi kutoka Hospitali ya Rufaa ya Njombe Bwana Marko Malaika amesema mafunzo hayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kwani kuna mambo kadhaa walikuwa hawayajui ila kwa sasa wataboresha zaidi ili jamii ipate huduma bora na salama.

Crever Mustapher ni Muuguzi kiongozi Njombe RRH Pamoja na kupongeza TNMC kwa kuwajengea uwezo katika utoaji huduma katika chumba cha upasuaji amesema kwa hatua waliyofikia kupata mafunzo hayo atahakikisha wauguzi na wakunga wote wanajengeana uwezo ili waweze kufahamu vyema namna ya kutoa huduma ya aina hiyo.

Sessilia Mtoro ambaye ni muuguzi kiongozi wa mkoa wa Njombe amekili kuwa kuna mambo mengi walikuwa wanafanya bila kufuata viwango vya utoaji huduma ila kwa sasa jamii itegemee huduma bora kutoka kwao baada ya kupata mafunzo hayo.

Ikumbukwe kuwa zaidi ya asilimia 80 ya watoa huduma za Afya hapa nchini ni wauguzi na wakunga ambapo hawa ndio wahudumu wanaoandaa chumba cha utoaji na vifaa tiba vitakavyotumika katika huduma ya upasuaji hivyo ni muhimu kwa wanataaluma hawa kujua hatua na taratibu za utoaji huduma ya aina hiyo.

# Watarajali Wapata Semina Elekezi Kabla ya Kuanza Mafunzo kwa Vitendo.



Na. Mwandishi wetu

Watarajali zaidi ya 700 wamekutana katika Ukumbi wa Chimwaga uliopo Jijini Dodoma tarehe 23.10.2024 kwa lengo la kupata semina elekezi kabla ya kuanza mafunzo kwa vitendo katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za Afya hapa nchini.

Semina hiyo iliyoandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania imelenga kuwajengea uwezo wakutoa huduma kwa kuzingatia kanuni,sheria na miongozo ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga hapa nchini.

Akizungumza na watarajali Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na ukunga hapa Nchini Bi. Ziada Sellah amewakumbusha watarajali hao kuzingatia taratibu za kiuuguzi na Ukunga sambamba na kuwataka kufanya tafiti katika kada hizo.

***"Sasa mmeshatoka vyuoni mnakwenda kuhudumia jamii nendeni mkahudumie jamii huku mkufanya tafiti za kutosha katika kada ya Uuguzi na Ukunga hatutegemei ninyi kukaa nyuma mmeandaliwa, mmeiva sasa nendeni mkafanye kazi"***- Bi. Ziada alisema.

Naye Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Mtawa amewasisitiza watarajali hao kuhakikisha wawapo katika maeneo ya kutolea huduma ni .

***"Nendeni mkahudumie jamii huku mkufanya tafiti za kutosha katika kada ya Uuguzi na Ukunga hatutegemei ninyi kukaa nyuma nyuma mmeandaliwa, mmeiva sasa nendeni mkafanye kazi"***

vyema kuzingatia miongozo ya sare ili kujitanabaisha baina ya wateja na wanataaluma wengine

***" Sisi zamani tulipo waona wauguzi na wakunga walituvutia kwa sare zao,unadhifu na mwonekano wao mpaka tukasema kazi si ndio hii sasa! Maana walivaa mavazi nadhifu na yenye kupendeza, nawaombeni mkifika huko mkazingatie usafi, sare kwa mujibu wa miongozo ya sare, hakikisheni mnazingatia hilo"*** -Bi. Agnes Mtawa.

Kwa upande wake Mrajisi wa Uuguzi na Ukunga kutoka Zanzibar Bwana Vuai Kombo Haji amewataka watarajali kuhakikisha wanakuwa na matumizi bora ya vifaa vyao vya mawasiliano sambamba na mitandao ya kijamii, huku akiwasisitiza kwenda kujifunza kwa vitendo.

Aidha, Mkurugenzi wa Maadili, usajili na leseni Bi. Jane Mazigo amewataka kuhudhuria siku zote zilizopangwa na Baraza bila ya kukosa ili kuhakikisha wanapata mafunzo mazuri ili kupata weledi wakutosha katika taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

Watarajali zaidi ya 700 wanatarajia kuanza mafunzo yao ya vitendo mwanzoni mwa mwezi wa kumi na moja katika vituo 29 hapa nchini

# Ujenzi wa Ofisi za TNMC Dodoma Wafikia 63%

**Na. Ezekiel Nyalusi**



Menejimenti ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) imetembelea eneo la ujenzi wa jengo la ofisi litakalokuwa makao makuu ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Oktoba Mosi, 2024 na kufanya kikao na mshauri mwelekezi TBA Pamoja na Mkandarasi kwa lengo la kuangalia maendeleo ya ujenzi wa Ofisi hizo.

Ujenzi huo unaotekelezwa na kampuni ya ujenzi ya Strategic Business Solution Limited (SBS) huku mkandarasi mshauri akiwa ni TBA, ujenzi huo unaoendelea katika eneo la Medeli Jijini Dodoma, Umefikia 63% huku ukigharimu kiasi cha Shilingi bilioni 1.8 za kitanzania.

Aidha, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania linajenga Ofisi Kuu Jijini Dodoma hii ni baada ya maelekezo ya Serikali ya kuzitaka Taasisi zote za Umma kuhamia Makao Makuu ya nchi, awali Ofisi kuu za TNMC zilikuwa Kibaha mkoani Pwani.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.






# TNMC yazindua Namba Mpya ya Huduma kwa Wateja.

Na. Mwandishi wetu



Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) 11.10.2024 limezindua mfumo wa mawasiliano ya huduma kwa wateja utakao tumika kuwasiliana na umma hususani wadau wake wakuu ambao ni wauguzi na wakunga ndani na nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha kilele cha wiki ya huduma kwa wateja.

Wiki ya huduma kwa wateja ilianza tarehe 07 Oktoba 2024 na kumalizika leo Oktoba 11, 2024 ikiwa imebeba kauli mbiu inayosema ***"Huduma zenye ubora na za kiwango cha juu zaidi".***

Akizindua mfumo huo wa mawasiliano katika ofisi za Baraza Jijini Dodoma kaimu Msajili Bi. Jane Mazigo, amesema kwa sasa Baraza litakuwa linatumia namba moja tu ya mawasiliano ili kuboresha utoaji huduma ameitaja namba hiyo maalum kuwa ni **0736 006060** ambayo itatumika kuwasiliana na Baraza kwa jambo lolote.

Bi. Mazigo ametanabaisha kuwa, namba hiyo itakuwa ikitumika muda na siku za kazi tu, ambazo ni Jumatatu hadi ijumaa kuanzia saa mbili kamili 02:00 asubuhi hadi 10:30 jioni.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.



# Chama cha "Wanafiziotherapia" cha Mtembelea Msajili TNMC

Ni mwandishi Wetu




Viongozi wa Chama cha "wanafiziotherapia" Tanzania (Association of Physiotherapists in Tanzania) leo oktoba 10,2024 wameitembelea ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Uunga Tanzania kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ya utendaji kazi wa TNMC.

Pamoja na mambo mengine mengi Viongozi hao ndg. Jerusalem Makotore(kulia) ambaye ni Mhazini na Dietrich Chussi (kushoto) ambaye ni katibu wameonesha kufurahia mapokezi hayo waliyoyapata kutoka ofisi ya Msajili.

Kaimu Msajili Bi. Jane Mazigo amewapongeza wataalam hao kwa kutembelea Ofisi ya Msajili na kuwaeleza namna Baraza linavyosimamia taaluma na kuhakikisha jamii inapata huduma bora aidha, amewakaribisha kwa wakati mwingine watakapohitaji kujifunza zaidi.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

**0736 00 6060**

**KWA MAWASILIANO NA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# HABARI PICHA



Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea wakaguzi kutoka Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi kwa lengo la kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.



Muuguzi Mkuu wa Serikali Bi. Ziada Sellah akizungumza na watarajali wakati wa semina elekezi iliyoandaliwa na TNMC iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chimwaga jijini Dodoma.



Msajili TNMC Bi. Agnes Mtawa, pamoja na maafisa waandamizi Salome Kassanga na Bi. Irene Chilewa katika Mkutano wa kisayansi wa ECSACONM nchini Lesotho



Msajili wa TNMC Bi. Agnes Mtawa akizungumza na watarajali wakati wa semina elekezi iliyoandaliwa na TNMC iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chimwaga jijini Dodoma.



Mwanasheria wa TNMC Geoge Shilla akizungumza na Watarajali wakati wa semina elekezi iliyoandaliwa na TNMC iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chimwaga jijini Dodoma.



Mkurugenzi wa Maadili,Usajili na leseni Bi. Jane Mazigo akizungumza na Watarajali wakati wa semina elekezi iliyoandaliwa na TNMC iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chimwaga jijini Dodoma.

# Tanzia

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Oktoba, 2024, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA: RHOBI KENYUKO MARO
KITUO: Hospitali ya Mpwawa
MKOA: Dodoma
WILAYA: Mpwapwa



JINA: JESCA KATAMBI
KITUO: Geita RRH
MKOA: Geita
Manispaa: Geita Mji



JINA: PAULO EMANUEL
KITUO: Hospitali ya wilaya
MKOA: Arusha
WILAYA: Arusha CC



JINA: VENANCIA CHARLES
MKOA: Dodoma
WILAYA: Dodoma Mjini.



JINA: JACOB B SANGA
KITUO: Korogwe DH
MKOA: Kagera
WILAYA: Korogwe Mji



JINA: JUSTINE A. FERNANDO
KITUO: Hospitali ya Mwambani
MKOA: Songwe

# Tanzia

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Oktoba, 2024, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA: HERENA JOHN
KITUO: Hospitali ya Wilaya
MKOA: Mbeya



JINA: TERESIA SIMFUKWE
KITUO: Hospitali ya H/W Kyela
MKOA: Mbeya



JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:** **0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA